**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# TANGAZO LA AJIRA YA WALIMU WA MKATABA WALIOCHAGULIWA NA KUPANGIWA KUFUNDISHA SOMO LA ELIMU YA BIASHARA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI

Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwa kushiriakiana na asasi ya Educate! Tanzania kupitia mradi wa kuboresha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Elimu ya Biashara (Business Studies), inatekeleza afua ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu ya Biashara (Business Studies). Ofisi ilitangaza nafasi 400 za walimu wa kujitolea (mkataba) wa somo la Elimu ya Biashara kwa ajili ya shule za Sekondari zenye uhitaji mkubwa, kwenye mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Simiyu, Kagera, Geita

Tabora, Dodoma, Morogoro, Pwani, na Dar es Salaam. Lengo la mradi huu ni kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 toleo la 2023 na Mtaala ulioboreshwa wa Elimu ya Sekondari unaoelekeza ufundishwaji wa somo la Elimu ya Biashara ili kuongeza ujuzi wa ujasiriamali kwa Wanafunzi.

Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI inatangaza Majina ya Walimu wa kujitolea kufundisha Somo la Elimu ya Biashara katika shule za sekondari waliokidhi vigezo, kuchaguliwa na kupangiwa shule za kufundisha kwa Mkataba. Walimu wote waliopangiwa shule za kufundisha wanatakiwa kufika katika Halmashauri husika kukamilisha taratibu za kuanza kazi kuanzia tarehe 24/07/2026 hadi tarehe 06/08/2026. Baada ya muda huo kupita, nafasi iliyo wazi itajazwa na mhitaji mwingine.

Majina ya Walimu wa kujitolea waliochaguliwa na kupangiwa shule za Sekondari za kufundisha somo la Elimu ya Biashara yanapatikana kupitia kiunganishi, **ajira.tamisemi.go.tz** na pia kupitia tovuti **www.tamisemi.go.tz**.

**Limetolewa na:**

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu -
TAMISEMI, Mji wa
Serikali - Mtumba,
S.L.P 1923,
**41185 DODOMA**